JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI

715 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

Muda: Saa 3:30 **Ijumaa, 17 Mei 2019 mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na saba (17)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A, maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B na maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

1 914715 100018

prof.exams.may19

Scanned by CamScanner

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. "Na (wakumbushe), Luqman alipomwambia mwanawe; na hali ya kuwa anampa nasaha, "Ewe mwanangu! Usimshirikishe Mwenyezi Mungu maana shirki ndiyo dhuluma kubwa"(31:13). Bainisha aina nne kuu za shirki.

2. Chambua vigezo vinne vya vazi la mwanamke wa Kiislamu.

3. Taja masharti manne kwa muoaji ili ndoa ya Kiislamu ikubalike.

4. Andika mafunzo manne yanayotokana na suratul- Ikhlas (112:1 – 4).

5. Bainisha maovu manne waliyojiepusha kufanya waislamu kutoka Yathrib katika mkataba wa kwanza wa A'qabah.

6. "Wenye taaluma mbalimbali wanategemewa kuwa wachamungu zaidi kutokana na taaluma zao". Nukuu aya mbili ndani ya Qur'an zinazothibitisha kauli hii.

7. Taja sehemu kuu mbili za muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu.

8. Onesha tofauti nne baina ya lengo kuu na lengo mahsusi katika ufundishaji wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

9. Orodhesha dondoo nne zinazoonesha umuhimu wa azimio la kazi la somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

10. Ainisha mambo manne muhimu ya kuzingatia wakati wa kutayarisha nukuu za somo.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii.

11. Na baadhi ya binadamu husema: "Je! Nitakapokuwa nimekufa, kweli nitafufuliwa kuwa hai (mara ya pili)?" (19:66-67). Kwa kuzingatia aya uliyopewa, ainisha hoja nne kuonesha uwezekano wa ufufuo.

12. Chambua mafunzo ya kuhuisha na kulinda Uislamu yanayopatikana kwa kufanya vitendo vinne vya Hija.

13. Eleza vipindi vikuu vinne vya historia ya uandishi wa Hadithi katika vitabu.

14. Elezea mbinu nne walizozitumia makafiri wa Makka kuupinga ujumbe aliokuja nao Mtume (s.a.w).

prof.exams.may19

Scanned by CamScanner

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

15. Eleza tofauti sita za msingi kati ya muhtasari na kitabu cha kiada katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu.

16. Bainisha madhara sita yatakayojitokeza ikiwa mwalimu wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu hatawapima wanafunzi wake mara kwa mara.

17. (a) Eleza maana ya zana za kufundishia.
    (b) Ainisha zana za aina tatu utakazozitumia kufundisha wanafunzi wa Kidato cha Kwanza kuadhini.

Scanned by CamScanner